ORAC SP/02

Ofisi ya Kamishna wa Maombi ya Ukimbizi

Oifig an Choimisinéara Iarratais do Dhideanaithe

Sheria za Mwaka 2013 (S.I. Na. 426 ya 2013) za Umoja wa nchi za Ulaya (hifadhi ya ulinzi wa ziada)

Utaratibu na mpangilio wa kuchunguza na kutoa uamuzi kuhusu maombi ya kupewa hifadhi ya ulinzi wa ziada

Taarifa na habari kwa waombaji wote

Taarifa na habari hii ni kwa ajili ya maelekezo tu. Haina lengo la kutoa tafsiri na maana ya sheria na taratibu hizi

1. Utangulizi

1.1 Taarifa hii inakupa maelezo kwa undani kuhusu sheria inayo tawala uchunguzi na uamuzi wa maombi ya kupewa hifadhi ya ulinzi wa ziada na serikali na dola yake kwenye Nchi za Muungano wa Nchi za Ulaya(hifadhi ya ulinzi wa ziada) Sheria za mwaka 2013 (S.I. Na. 426 ya 2013)-(Sheria za mwaka 2013)

1.2 Sheria za mwaka 2013 zilitengenezwa na Waziri wa Haki na Usawa(Waziri) na zilianza kutumika mnamo tarehe 14 November 2013 (tarehe ya kuanza kutumika)

1.3 Kwa mujibu wa sheria za mwaka 2013, ushughulikiaji wa kupewa hifadhi ya ziada ya kulindwa umewekwa na kuwa jukumu la Kamishna wa Maombi Ukimbizi (Kamishna)

1.4 Ni muhimu na ni kwa manufaa na faida yako kusoma maelezo haya na taarifa hizi kwa makini kabisa ili ujue kwa uhakika mambo muhimu yafuatayo:

(i)Haki zako, wajibu na majukumu yako wakati ukiwa hapa Ireland katika kipindi unangoja uamuzi wa maombi yako ya kupewa hifadhi ya ziada ya kulindwa

Utaratibu chini ya sheria za mwaka 2013 ambazo ndizo zitatumika katika hatua za uamuzi wa wewe kupewa hifadhi ya ziada kwa ajili ya usalama.

(ii)Umuhimu wa kufuata bila kukosa mipaka ya muda na matakwa mengine yaliyowekwa chini ya sheria za mwaka 2013 na kujibu mara moja kwa wahusika inapotakiwa katika kila hatua ya maombi haya.

1.5 Kama utahitaji taarifa na maelekezo zaidi, kutokana na kesi au hali uliyonayo binafsi ushauri wa kisheria utapatikana.

2. Lengo la Sheria za mwaka 2013

2.1 Sheria hizi zinatoa utaratibu na mfumo mzima wa kuchunguza, na kuamua kuhusu maombi ya hifadhi ya ziada katika nchi na dola hii kutoka na baada ya tarehe 14 mwezi wa kumi na moja, Novemba, mwaka 2013.

2.2 Pia sheria hizi zitatumika kuamua kuhusu maombi ya hifadhi ya ulinzi wa ziada yalifanywa kwa waziri wa Haki na Usawa(kitengo cha Uhamiaji na kupewa uraia wa Ireland) ambayo hayajatolewa uamuzi bado kabla ya tarehe ya kuanza kutumika sheria mpya za mwaka 2013 yaliyohamishiwa kwa Kamishna kuangaliwa kutoka tarehe hiyo.

3. Sheria za mwaka 2013 zinahusu na kushughulika na mambo yapi?

Kama wewe ndiyo unafanya maombi ya hifadhi ya ulinzi wa ziadi kwa mara ya kwanza:

3.1 Sheria za mwaka 2013 inasema kwamba kutoka mwezi wa kumi na moja, Tarehe 14 Novemba, 2013 maombi ya mtu kupewa hifadhi ya ulinzi wa ziada yatachunguzwa na kufanyiwa uamuzi na Kamishna.

3.2 Kutoka tarehe hii, maombi mapya ya kupewa hifadhi ya ulinzi wa ziada yanaweza kupelekwa kwa wa Waziri wa Haki na Usawa, lakini maombi lazima yajazwe kwenye fomu sahihi kwa Kamishna. Kamishna baada ya kumfanyia muhusika usahili

wa kumuuliza maswali ana kwa ana kuhusu kupewa hifadhi ya ulinzi wa ziada ataandaa taarifa ya maandishi kuhusiana na uchunguzi wa ombi hilo. Kamishna atatoa ushauri kwa Waziri wa Haki na Usawa kuhusu maombi ya muhusika kupewa hifadhi ya ulinzi wa ziada au hapana.

Kama wewe <u>ulishafanya na kutuma</u> maombi ya kupewa hifadhi ya ulinzi wa ziada na maombi yako <u>hayajajibiwa</u> bado na Waziri:

3.3 Maombi ya kupewa hifadhi ya ulinzi wa ziada ambayo yalikuwa <u>hayaja amuuliwa na kujibiwa bado</u> na Waziri wa Haki na Usawa kabla ya tarehe ya kuanza kutumika sheria za mwaka 2013 yaliyohamishiwa kwa Kamishna kwa uchunguzi na kutolewa uamuzi. Waziri atawatumia taarifa watu wote waliofanya na kutuma maombi ya hifadhi ya ulinzi wa ziada kuhusu mpangilio na utaratibu mpya kuhusu namna na jinsi maombi yao yatakavyotolew uamuzi.

3.4 <u>Watu wote ambao walishafanya maombi ya kupewa hifadhi ya ulinzi wa ziada hawahitaji kufanya maombi mapya ya kupewa hifadhi ya ulinzi wa ziada kwa Kamishna lakini wanaweza kutoa na kuleta maelezo zaidi kwa Kamishna kuhusiana na maombi yao (angalia kifungu 7.5 hapo chini)</u>

4. Nini maana ya hifadhi ya ulinzi wa ziada?

4.1 Hifadhi ya Ulinzi wa Ziada ni ulinzi unaotolewa kwa mtu ambaye imethibitika na kutambuliwa kuwa kuna misingi ya kutosha ya kuamini kuwa mtu anayehusika, kama akirudishwa kwenye nchi yake ya asili, atakutana na kukabiliana na hatari ya kweli ya kupata madhara na mambo makali ya kudhumdhuru au kutokana na hatari hizo mtu huyu hapendi kurudi na kupewa ulinzi wa nchi yake. Mtu huyu anapashwa na lazima awe ambaye hazuiliwi na sheria kuomba hifadhi ya ulinzi wa ziada.

4.2 Madhara na mambo <u>makali</u> ya kudhumdhuru ina maana hii: –

(a) adhabu ya kifo au kuuawa; au

(b) mateso au kufanyiwa mambo yasiyo ya kibinadamu au mambo asiyopaswa kufanyiwa mtu au mtu kuadhiwa kwenye nchi yake ya asili; au

(c) vitisho vikali vya maangazi ya watu binafsi na raia au mtu kutokana na maangamizi katika hali ya vita ya taifa na au mataifa au vita ya ndani ya nchi yenyewe kati ya watu wa nchi hiyo.

4.3 Kama unastahili kupewa hifadhi ya ulinzi wa ziada utaruhisiwa kubaki katika nchi na dola hii na utakuwa na haki Fulani za msingi, Haki hizi zimeandikwa kwenye Sheria za mwaka 2013.

5. Nani anawestahili kupewa hifadhi ya ulinzi wa ziada?

5.1 Kama na Maadamu upo hapa katika nchi hii, unastahili na una haki ya kuomba hifadhi ya ulinzi wa ziada kadri na kutokana na sheria za mwaka 2013 kama:

(a) wewe siyo raia na hujapewa uraia wa Nchi za Umoja wa Nchi za Ulaya,
(b) Kama maombi yako ya kupewa ukimbizi yamekataliwa hapa Ireland,
(c) Kuna msingi na uthibitisho wa kutosha ulionyeshwa na kukubalika kuamini na kuthibitisha kuwa kama utarudishwa kwenye nchi yako asili, utapata matatizo na kukutana na kukabiliana na hatari kali za kukudhuru na kuhatarisha maisha yako, na kuwa huwezi au kutokana na hatari hizo hupendi kurudi na kuomba nchi yako ya asili ikulinde kama raia yeyote wa nchi yako na,
(d) wewe hukataliwi na kuzuiwa na sheria kuomba hifadhi ya ulinzi wa ziada.

5.2 Utazuiwa na kukataliwa kuomba ulinzi wa ziada kutokana na sheria za mwaka 2013 kama kuna sababu za msingi, nzito na kutosha kusema na kuthibitisha kuwa –

(a) kuwa umefanya makosa na uhaini dhidi ya amani, makosa na uhaini yanayokataliwa kufanywa vitani, au umefanya makosa na uhaini dhidi ya binadamu na ubinadamu kama inavyotafsiriwa na sheria za kimataifa znazotoa sheria dhidi ya makosa haya;
(b) umefanya makosa makali ya ukiukaji wa sheria;
(c) umefanya makosa kinyume cha malengo na kanuni za Umoja wa Mataifa kama ilivyoandikwa kwenye utangulizi katika kifungu cha cha kwanza 1 na kifungu cha pili 2 cha katiba ya Umoja wa Mataifa au,
(d) Wewe ni hatari kwa jamii na usalama wa nchi hii.

5.3 Hutakubaliwa kuomba ulinzi wa ziada kama:

(i) kuna sababu nzito za kufikiria kuwa umesababisha na kuchochea au umeshiriki katika kufanya makosa au matendo yanayohusiana na makosa yaliyoandikwa kwenye kifungu cha 5.2 (a) mpaka (d),

(ii) umeondoka nchini kwako kwa sababu tu ya kukimbia na kuzuia kuathibiwa kwa kosa au makosa (lakini siyo makosa au matendo yanahusiana na makosa yaliyoandikwa kwenye kifungu cha 5.2 (a)mpaka (d), makosa ambayo hukumu yake ni kwenda jela katika nchi hii ambayo utakuwa umeyafanya kabla hujaingia katika nchi na dola hii .

6. Nani anaweza kuomba hifadhi ya ulinzi wa ziada?

6.1 Kwa kuzingatia sheria za mwaka 2013, maombi ya ulinzi wa ziada yanaweza kufanywa na mtu ambaye:

(i) Yupo hapa katika nchi hii,
(ii) Maombi yake ya kuwa mkimbizi yamekatawaliwa hapa Ireland.

6.2 Kama Waziri ataamua usipewe ukimbizi utapewa taarifa kwa maandishi kuwa maombi yako ya kupewa ukimbizi yamekataliwa .

6.3 Taarifa ya kukataliwa usipewe ukimbizi itakuja na maelezo kuhusu maombi ya kupewa hifadhi ya ulinzi wa ziada na fomu yake yakuombea hifadhi hiyo. Kama unafikiria unastahili kuomba hifadhi ya ulinzi wa ziada itabidi ujaze fomu na kuileta kwa Kamishna ndani ya siku kumi na tano, 15 za kazi kutoka siku walipotuma taarifa ya wewe kutaliwa kupewa ukimbizi.

7. Maombi yangu ya kupewa hifadhi ya ulinzi wa ziada yatachunguzwa na kufikiriwa vipi na Kashmina wa Maombi ya Ukimbizi?

7.1 Maombi yako ya kupewa hifadhi ya ulinzi wa ziada yatachunguzwa na kuamuliwa na Kamishna kadiri ya sheria za mwaka 2013.

7.2 Chini na kwa kufuata utaratibu mpya wa kushughulikia maombi ya kupewa ulinzi wa ziada utatakiwa kuja na kuhudhuria usahili ambapo utaulizwa maswali ana kwa ana kuhusu maombi yako ya kupewa hifadhi ya ulinzi wa ziada. Lengo la usahili huu ni kutaka kupata maelezo yote na kamili kuhusu maombi yako ya hifadhi ya ulinzi wa ziada.

7.3 Mwombaji lazima aje na kuhudhuria usahili wa kuulizwa maswali katika Ofisi ya Kamishna wa Maombi ya Ukimbizi katika siku, tarehe na muda aliopangiwa kuja kuulizwa maswali ana kwa ana. Muombaji asipokuja na kuhudhulia usahili katika siku na muda aliopewa maombi yake yatahesabiwa kuwa ameyasitisha(Angalia kifungu 8.2)

7.4 Mwombaji anaweza kufanya kuleta na kuwasilisha kwa Kamishna kitu chochote kwa njia ya maandishi kuhusiana na maombi yake wakati ombi lake linachunguzwa na kufikiriwa, na Kamishna atalichukulia jambo liloletwa kwake kwa maandishi kabla na wakati wa usahili wa kuulizwa maswali ana kwa ana chini ya sheria za mwaka 2013. Pia uwasilishi na uletaji wa mambo kwa Kamishna wa ukimbizi unaweza fanywa na Kamishna wa Umoja wa Mataifa wa Wakimbizi(United Nations High Commissioner for Refugees-UNHCR) au mtu yeyote anayehusika.

7.5 Kama wewe tayari umefanya maombi ya kupewa hifadhi ya ulinzi wa ziada na maombi yako bado hayajatolewa uamuzi wakati sheria mpya za mwaka 2013 kabla hazijaanza kutumika,unaombwa na unatakiwa kusoma maelezo ya maelekezo yaliyotumwa na barua kwako na ofisi ya Uhamiaji na Uraia (Naturalisation and Immigration Service) kuhusu wewe kuleta na kuwasilisha maelezo zaidi pamoja na nyaraka na hati zozote nyingine kwa Kamishana.

7.6 Kila wakati itakapokuwa lazima ili kuhakikisha kunakuwa na mawasiliano mazuri wakati wa usahili wa wewe kuulizwa maswali ana kwa ana kuhusu maombi yako, kuwe na mtu wa kutafsiri kutoka lugha yako unayotaka atatolewa na Kamishna.

Mtiririko wa hatua za kushughulikia maombi

7.7 Ufuatao hapo chini ni mlolongo wa utaratibu wa kushughulikia maombi ya kupewa hifadhi ya ulinzi wa ziada.

(i) Kamishna atapanga wewe kuja kufanyiwa usahili, yaani kuulizwa maswali ana kwa ana kuhusu maombi yako.

(ii) Baada ya usahili wa wewe kuulizwa maswali ana kwa ana , taarifa itaandaliwa kuhusu majibu ya uchunguzi wa maombi yako na uamuzi uliotolewa na Kamishna kwa Waziri wa Haki na Usawa kama wewe unastahili kupewa hifadhi ya ulinzi wa ziada.

(iii) Ikitokea kuwa majibu yamekataa usipewe hifadhi ya ulinzi wa ziada, utakuwa na haki kupinga majibu yaliyotolewa kwenye Mahakama ya Kukata Rufaa ya Wakimbizi(Refugee Appeals Tribunal) ndani ya siku kumi na tano 15 za kazi kutoka siku na tarehe yalipotumwa majibu ya Kamishna kutaa usipewe hifadhi ya ulinzi wa ziada..

(iv) Kwa kuzingatia maelekezo ya Kamishna au uamuzi wa Mahakama ya Rufaa ya Wakimbizi, Waziri kwa kufuata sheria za mwaka 2013 atakubali upewe au atakataa usipewe hifadhi ya ulinzi wa ziada .

7.8 Ikiwa maombi yako ya kupewa hifadhi ya ulinzi wa ziada yatakuwa yamekataliwa utatumiwa taarifa ya maandishi inayosema:

(a) Maombi yako ya kuomba hifadhi ya ulinzi wa ziada yamekataliwa;

(b) Kipindi cha muda wako kubaki hapa katika nchi na dola hii umekwisha;

(c) waziri anapendekeza kutoa amri ya wewe kuchukuliwa na kuondolewa hapa katika nchi hii chini ya kifungu cha 3 cha Sheria ya Uhamiaji ya mwaka 1999.

(d) Una uwezekano na haki ya kupeleka maombi na taarifa nyingine kwa maandishi kwa waziri ndani ya siku kumi na tano, 15 za kazi, ukieleza kwanini unaomba uruhusiwe kuendelea kukaa katika nchi na dola hii.

8. MUHIMU: Je ninaweza kuachisha, kusitisha na kurudisha maombi niliyofanya tayari na Je maombi yangu kweli yatasitishwa na kurudishwa?

8.1 Maombi ya kuomba hifadhi ya ulinzi wa ziada yanaweza kusitishwa na kusimamishwa na mwombaji kwa kutuma taarifa ya maandishi ya kusitisha maombi hayo kwa Kamishna.

8.2 Pale ambapo muombaji hakuja na kuhudhuria usahili katika siku aliyopangiwa na Kamishna, na labda kama mwombaji atatoa maelezo kwa Kamishna katika siku tatu

tu za kazi kutoka tarehe aliyokosa kuja kwa usahili, maombi yake ya kupewa ulinzi wa ziada yatahesabika kuwa yamesitishwa kutokana na sheria za mwaka 2013.

8.3 Pale inapooneka na Kamishna kuwa mwombaji:

(i) Anashindwa katika wajibu wake na jukumu lake la kushirikiana na Kamishna wakati maombi yake ya ulinzi wa ziada yachunguzwa na kutazamwa au

(ii) anashindwa katika wajibu na jukumu lake la kutoa taarifa zinazohusu maombi yake ya kupewa ulinzi wa ziada, au

pale ambapo Waziri atamuarifu Kamishna kuwa ana maoni kuwa mwombaji amevunja na kukiuka wajibu wake:

(iii) kutoondoka au kujaribu kuondoka katika nchi na dola hii bila ridhaa na kukubali kwa Waziri, au

(iv) kumuarifu na kumweleza Kamishna anuani na mahali anapokaa au mabadiliko ya anuani na mahali anapokaa mapema inavyowezekana,

Kamishna atamtumia mwombaji taarifa kwa maandishi kumwomba na kumualika katika na ndani ya siku kumi na tano 15 za kazi tangu atakapomtumia barua hiyo, mwombaji aseme kama anapenda kuendelea na maombi yake ua hapana, na kama mwombaji hata sema katika muda huo ulipangwa na aliopewa, maombi yake kupewa hifadhi ya ulinzi wa ziada yatahesabiwa na kuchukuliwa kuwa yameachwa au yamesitishwa na kuwa mwombaji hapendi kuomba tena huo hifadhi ya ulinzi wa ziada kadiri ya sheria za mwaka 2013. Taarifa ya Kamishna kuhusiana na maombi ya namna hii itatoa ushauri pia kuwa mwombaji anayehusika asitambulike kama mtu anayestahili hifadhi ya ulinzi wa ziada.

8.4 Pale ambapo maombi ya hifadhi ya ulinzi wa ziada yamesitishwa au yameonekana kuwa yamesitishwa hakutakuwa na kukata rufaa kwenye Mahakama ya Rufaa ya Wakimbi.

9. Jinsi ya kupata taarifa na habari kuhusu hatua za kuomba na ushughulikiaji wa maombi ya kupewa hifadhi ya ulinzi wa ziada

9.1 Sheria za mwaka 2013 zinapatikana kwenye tovuti ya Kamishna wa Maombi ya Ukimbizi hapa http://www.ORAC.ie.

9.2 Taarifa na habari hizi zinapatikana katika lugha mbalimbali kwenye tovuti hii ya Kamishna wa Maombi ya Ukimbizi.

10. Taarifa na habari nyingine

10.1 Una haki ya kuomba ushauri kwa mwanasheria na unaweza kupata huduma za Shirika la Huduma za Kisheria kwa Wakimbizi, (Refugee Legal Service-RLS) kuhusu maombi yako ya kupewa ulinzi wa ziada. Shirika la Huduma za Sheria kwa Wakimbizi ni shirika huru kabisa linatoa huduma kwa wanaomba ukimbizi na halitoi taarifa kwa mtu au serikali, linafanya kazi kwa faida ya waomba ukimbizi tu na si serikali au mtu mwingine.

10.2 Una ruhusa na unakubaliwa kubakia katika nchi na dola hii mpaka uamuzi wa mwisho utapotolewa na kupatikana kuhusu maombi uliofanya. Waziri atawapa waombaji wote barua kuhusu maombi yao. Waombaji wapya watapokea barua hii kutoka kwa Kamishana.

10.3 Sheria za mwaka 2013 zinatakiwa zisomwe na kuangaliwa kwa masuala ya kujua mambo utaratibu na mpangilio mzima ambayo hayajaandikwa kwenye waraka na taarifa hii unayosoma na maelezo ya haki za mwombaji anayestahili kuomba hifadhi ya ulinzi wa ziada na ambaye sheria za mwaka 2013 za hifadhi ya ulinzi wa ziada zinatumika kwake.

Taarifa kwa waombaji walituma maombi yao na ambao maombi yao <u>bado hayatolewa</u> uamuzi na majibu na Waziri wakati wa kuanza kutoka kwa sheria hizi mpya

10.4 Kama wakati wa kuanza kutumika kwa sheria mpya za mwaka 2013 ulikuwa tayari umefanya maombi ya kupewa hifadhi ya ulinzi wa ziada na bado uamuzi haujafanywa na majibu kutolewa kuhusu na juu ya maombi yako inabidi ufuate na uzingatie yafuatayo:

- Kamishna atawasiliana na wewe katika muda si murefu kuhusu kupanga usahili wa wewe kwenda kuulizwa maswali, kwa hiyo hakuna haja au hitajiko la wewe kuwasiliana na Ofisi ya Kamishna wa Maombi ya Ukimbizi(Office of Refugee Application Commissioner –ORAC) moja kwa moja au namna nyingine na

- Kama haupo katika hatari ya kuchukuliwa, kuondolewa na kurudishwa nchini kwenu kutoka hapa katika nchi hii.

14 November 2013

ANWANI ZA OFISI MUHIMU HUSIKA

Ofisi ya Kamishna wa Maombi ya Ukimbikizi
(Office of the Refugee Applications Commissioner)
Timberlay House,
79-83 Lower Mount Street,
Dublin 2.

Simu: 01 6028000
Simu ya bure: 1890 202 418
Tovuti : www.orac.ie
E- mail: oracmail@orac.ie

Mahakama ya Kukata Rufaa kwa wakimbizi
(Refugee Appeals Tribunal)
6/7 Hanover Street East,
Dublin 2.

Simu: 01 4748400
Simu ya bure: 1890 201 458
Tovuti: www.refappeal.ie
E-mail: info@refappeal.ie

Ofisi ya Shirika la Msaada wa Sheria kwa wakimbizi
Refugee Legal Service Law Centre - Smithfield,
Kituo cha msaada wa Sheria kwa wakimbizi
48/49 North Brunswick Street,
Georges Lane,
Dublin 7.

Simu: 01 646 9600.
Tovuti: www.legalaidboard.ie
Email: lawcentresmithfield@legalaidboard.ie

Shirika la Kimataifa la Uhamiaji
International Organisation for Migration (IOM)
116 Lower Baggot Street,
Dublin 2.

Simu ya bure: 1800 406 406
Simu: 01 6760655
Website: www.ireland.iom.int
Email: iomdublin@iom.int

Kamishna wa Umoja wa Mataifa wa Wakimbizi
United Nations High Commissioner for Refugees (UNHCR)
Suite 4,
Merrion House,
1-3 Lower Fitzwilliam Street, Dublin 2.

Simu: 01 6314510.
Tovuti: www.unhcr.ie.
E-mail: iredu@unhcr.org.